Toleo 61 - Jumada II 1443 AH / Februari 2021 M

# Jarida la UQAB

**TAARIFA KWA VYOMBO VYYA HARABI**
Taasisi za Fedha za Kimataifa Zinafanyia Kazi Ajenda ya Kiunyonyaji

**HABARI NA MAONI**
Dori ya Dini katika Enzi ya Mfumo wa Kirasilimali wa Kisekula

**TOLEO JIPYA**
Dola ya Tashwishi ya Kirasilimali Ikivalia Vazi la Kiislamu

**JIBU LA SWALI**
Kwa Nini Mtume (saw) Hakuomba Nusra (Nguvu za Kimada) kutoka kwa Maquraish



## Uchochezi na uenezaji wa sumu za Kikabila ni Ada ya siasa ya Kidemokrasia iliofeli

Afisi ya Habari
ya Hizb ut Tahrir
Kenya

بسم الله الرحمن الرحيم

﴿وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا ۚ يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا ۚ وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ﴾

KUMB: 06/1443 | Jumatano, 09 Jumada II 1443 H | 12/01/2021 M

**Taarifa kwa Vyombo Vya Habari**

# Uchochezi na uenezaji wa sumu za Kikabila ni Ada ya siasa ya Kidemokrasia iliofeli

Seneta wa Meru anakabiliwa na mashtaka ya madai ya matamshi ya uchochezi aliyoyatamka kwenye mkutano wa kisiasa wa naib rais William Ruto huko Eldoret. Kwengineko mkurugenzi mkuu wa mashtaka ya umma amemwaagiza mkuu wa Polisi Hillary Mutyambai kumchunguza mbunge wa eneo la kitutu chahe huku Kisii Richard Onyoka kwa matamshi aliyoyasema kwenye mkutano wa kisiasa. Kulingana na baadhi ya ripoti mbunge huyo alikamatwa kwa mashtaka ya kutamka semi za chuki za kuchochea ghasia. Tuhuma hizi za matamshi ya kiuchochezi ndizo za karibu zaidi kuripotiwa humu nchini hali ambayo sasa imekua ada ya siasa za Kenya.

Miezi saba kufikia kwenye uchaguzi mkuu, tayari hali ya kisiasa nchini inaanza kugubikwa na taharuki na uchochezi kwenye safu za wanasiasa. Viongozi wa kisiasa wakijitolea kwa udi na uvumba kujaribu kuyafikia maslahi yao ya kisiasa, kiuchumi na na kijamii kwa kutumia mbinu ya kuwabagua raia kimaeneo sambamba na kueneza sumu za ukabila ambazo hutumiwa kama zana zao za kufikia malengo yao ya kisiasa. Kwa kutumia mbinu hizi chafu, wanasiasa wa mirengo yote husikika wakitamka semi za uchochezi na kupandikiza ukabila.

Kwa kuwa Demokrasia ni siasa ya ‘wengi wape’ hali inayopelekea wanasiasa wake kuweza kuunda na kubuni miungano ya kikabila na kimaeneo itakayowawezesha kupata kura nyingi. Miungano ya kikabila ndio kiashirio kikubwa kwenye mashindano ya kuingia ikulu- nafasi kubwa ya kisiasa ya nchi. Kwa kuwa msingi wa itikikadi ya kiilmaaniya (secularism) umefanya kipimo cha matendo ya wanadamu ikiwemo siasa ni kujitafutia mapato na maslahi hivyo siajabu kusikia ule msemo maarufu wa kisiasa usemao: “**Hakuna adui wa kudumu wala rafiki wa kudumu bali yaliyoko ni maslahi ya kudumu.**” Itikadi hii ndio hupelekea kuibuka kwa ndoa na miungano mpya za kisiasa kwenye kila muhula wa uchaguzi, ambayo wanasiasa hulenga kushinda tu uchaguzi wala sio kuhudumikia jamii.

Tungependa kueleza bayana kwamba mfumo huu wa Kidemokrasia unaotawala leo duniani umeshindwa kudhamini mabadiliko ya kiutawala ya amani na utulivu kutoka uongozi mmoja hadi kwa mwengine. Isitoshe,mfumo huu kimaumbile huzua hofu na taharuki miongoni mwa raia hasa katika vipindi vya uchaguzi na hili si tu kwa Kenya tu bali hata zile nchi zinazojipiga kifua kuwa zimeendelea Kidemokrasia kama vile Marekani. Ikumbukwe kwa mfano, Januari mwaka jana mashindano ya kisiasa kati ya Biden na Trump yaligeuka fujo pale wafuasi wa Trump walipovamia jengo kuu la Capitol Hill. Si hilo tu bali khiyana za Kisiasa nazo zimekua mmoja wapo ya sifa inayojitokeza katika siasa ya Demokrasia ambapo maslahi yakiwa ni yenye kuzunguka kadri ya mazingira ya kisiasa yanapobadilika.

Uislamu una mfumo wa kiutawala wa aina yaka uliokitia kwenye msingi wa kuchanganya hisia ya kiroho (Uchamungu) katika matendo yote yakiwemo ya kisiasa. Kwa mantiki hii, ndio michakato yote ya kisiasa ipo katika kutafuta radhi za MwenyeziMungu (swt). Sifa ya uchajimungu humfanya mtu yoyote akiwemo kiongozi wa kisiasa kufanya uongozi na siasa kuwa ni ubebaji wa majukumu na uwajibikaji asili ukilenga ufanisi sio tu maisha ya hapa duniani bali hata kesho akhera. Kwa msingi wa falsafa hii, Uislamu ukazalisha wanasiasa wakomavu na mahiri walio na sera imara zilizopelekea kuweko na ufanisi wa kisiasa, kiuchumi na kijamii kama ilivyoshuhudiwa katika kipindi cha utawala wa Khilafah kwa karne kumi na tatu.

**Shabani Mwalimu**
**Mwakilishi Kwa Vyombo Vya Habari, Hizb ut Tahrir Kenya**



**Email: info@uqab.or.ke**

بِسۡمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحۡمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ

﴿وَعَدَ ٱللَّهُ ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ مِنكُمۡ وَعَمِلُواْ ٱلصَّٰلِحَٰتِ لَيَسۡتَخۡلِفَنَّهُمۡ فِي ٱلۡأَرۡضِ كَمَا ٱسۡتَخۡلَفَ ٱلَّذِينَ مِن قَبۡلِهِمۡ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمۡ دِينَهُمُ ٱلَّذِي ٱرۡتَضَىٰ لَهُمۡ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّنۢ بَعۡدِ خَوۡفِهِمۡ أَمۡنٗاۚ يَعۡبُدُونَنِي لَا يُشۡرِكُونَ بِي شَيۡـٔٗاۚ وَمَن كَفَرَ بَعۡدَ ذَٰلِكَ فَأُوْلَٰٓئِكَ هُمُ ٱلۡفَٰسِقُونَ﴾

Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir Tanzania

حزب التحرير
Hizb ut Tahrir

KUMB: 02/1443 | Ijumaa, 27 Jumad I 1443 H | 31/12/2021 M

Taarifa kwa Vyombo Vya Habari

# Taasisi za Fedha za Kimataifa Zinafanyia Kazi Ajenda ya Kiunyonyaji

Katika kipindi kisichozidi mwaka mmoja tangu kushika mamlaka ya uraisi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Rais Samia Suluhu tayari serikali imeshachukua mkopo wa kiasi cha billioni $3 ikihusisha kinachoitwa mifuko ya mikopo yenye takhfifu na pia kutoka katika mfuko wa kujifariji na majanga kutoka Benki ya Dunia, Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB).

Benki ya Dunia pekee imeikopesha Tanzania mkopo wa kiasi cha billioni $2.29 kwa ajili ya miradi mbali mbali ikiwemo millioni $500 kwa ajili ya kutoa msukumo wa Mpango wa Masomo ya Elimu ya Msingi, millioni $150 kwa ajili ya Mradi wa Kuimarisha Umilikishaji Ardhi (LTIP) na millioni $500 kwa ajili ya Mradi wa kuboresha Kiwango cha Elimu ya Sekondari Tanzania.

Nayo IMF iliidhinisha kiasi cha millioni $567 kwa Tanzania, miongoni mwao millioni $189 kutoka chini ya Mpango wa Mikopo ya Kiharaka na millioni $378 chini ya Mpango wa Ufadhili wa Kiharaka.

Pia, Tanzania imechukua mkopo wa kiasi cha millioni $256 kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika, huku kiasi cha millioni $140 kikilengwa kutumika katika uzalishaji wa nishati ya umeme na mtandao wa uunganishaji wake, ilhali kiasi cha millioni $116 kitatumika kwa ajili ya maboresho makubwa ya barabara ya kilomita 160 inayounganisha Mnivata- Newala na Masasi, kusini mwa Tanzania.

Tanzania kama zilivyo nchi nyengine za Afrika imekuwa ikikopa kutoka kwa taasisi hizo za kimataifa kwa miaka mingi tu, wala hakuonekani dalili ya kusita wala hali ya kujisimamia mambo yake kwa kuwa huru kutokana na madeni na ukopaji huo.

Mfano hai, ndani ya mwaka 2015, deni la Tanzania lilkuwa trillioni 35 na hadi kufikia Aprili 2021 limeshapaa kufikia trillioni 60.9. Hali hiyo imejiri kutokana na kuchukua mikopo kutoka kwa taasisi hizo za kifedha za kimataifa.

Tangu Marekani itamalaki kimataifa baada ya Vita vya Pili vya Dunia iliasisi mpango mpya kabambe wa kudhibiti uchumi kufuatia Mawafikiano ya Bretton Woods ndani ya mwaka 1944, kutokana nayo iliundwa Benki ya Dunia na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF), taasisi mbili hizo zikiwa ala muhimu za Marekani kudhibiti uchumi, ikizitumia kama kadi yake ya kuchezea uchumi, na baadhi ya wakati kupitia mikopo ili kuondoa tawala ambazo awali zilikuwa vibaraka wa mabwana wa ukoloni mkongwe (Uingereza na Ufaransa) na kuzibadilisha tawala hizo kuwa vibaraka wake wapya. Pia taasisi mbili hizo hutumika kuwa na udhibiti kikamilifu wa uchumi wa nchi mbali mbali kupitia makampuni ya Marekani ya kimataifa, ikipelekea wizi wa vyanzo vya uchumi vya nchi mbali mbali kwa kubadilisha mali za Umma kuwa za kibinasi chini ya ajenda yake ya ubinafsishaji nk.

Kwa hivyo, taasisi zote za kifedha za kimataifa iwe Benki ya Dunia, IMF, za Ulaya, za China au hata Benki ya Maendeleo ya Afrika iliyoasisiwa mwaka 1964, zote hizo si chochote si lolote ila kimaumbile ni taasisi za kibepari ambazo kamwe hazikudhamiriwa kuisaidia Afrika au nchi zinazoendelea. Lakini kimsingi zina ajenda ya kiunyonyaji zikilazimisha kwa ukatili na bila ya huruma sera za kinyonyaji kama Sera ya kufanya mabadiliko ya kimuundo iliyoleta mashaka na maangamizi makubwa kwa uchumi na watu.

***Endelea... UK 4***

Kwa sasa inadhihirika wazi kwamba madeni ni ala ya kinyang'anyiro cha ukoloni mambo leo baina ya Marekani, Ulaya na China ili kutenza nguvu na kunyonya mrundikano mkubwa wa rasilimali za Afrika na utajiri wake kupitia baraka za wanasiasa wa nchi zinazoendelea kwa gharama ya wananchi wanyonge ambao ndio wahanga wakubwa wa maumivu ya madeni hayo na wabebaji mzigo wa kodi ili kulipia madeni hayo. Katika baadhi ya nchi zinazoendelea wamefikia hatua ya kupoteza miundombinu yao nyeti kwa kushindwa kulipa madeni makubwa ya nje kwa wakati. Orodha ya nchi zilizosibiwa na hali hiyo ni ndefu, zikiwemo nchi kama Zambia, Uganda Sri Lanka nk.

Mataifa ya nchi zinazoendelea ikiwemo Tanzania lazima ziamke kwamba ulimwengu unahitaji mfumo wa uadilifu wa Uislamu ili kuwa na maamiliano ya kiuadilifu ya kiuchumi, na sio mfumo muovu na wa kiunyonyaji wa Ubepari. Uislamu chini ya utawala wake wa Khilafah utauokoa ulimwengu na ubinadamu kiujumla kutokana na minyororo yote ya kiunyonyaji.

**Masoud Msellem**

**Mwakilishi kwa Vyombo vya Habari, Hizb ut Tahrir Tanzania**

# HABARI NA MAONI
# Dori ya Dini katika Enzi ya Mfumo wa Kirasilimali wa Kisekula

**Habari:**

Kasisi Ssebagala alitoa maagizo yafuatayo mnamo Jumamosi katika Kanisa la St Paul Kanjuki katika Wilayah ya Kayunga alipokuwa akitoa mkono wa kuwaaga Wakristo kabla kustaafu kwake mwaka huu. “Walimu wakuu wote, nataka kuwaambia kwamba hatutoruhusu wasichana wenye mimba au wanaonyonyesha darasani. Wasichana wote wakija, fanyeni ukaguzi wa kawaida wa kimatibabu ili wale watakaopatikana kuwa wana mimba waweze kurudishwa ili wakazae watarudi baada ya kujifungua.” Kwa kuongezea, alisema, “Chukulia mtu anayesema kuwa wanaonyonyesha waruhusiwe darasani. La, hili hatutolikubali kwa sababu shule zetu zilianzishwa kwa ajili ya kutoa maarifa bali hata pia kuwapa watoto nidhamu. Inawezekanaje kwa mwalimu kuwa anafundisha ilhali msichana anampa matiti mwanawe?”

Katika kujibu matamshi yaliyotolewa na kasisi, Waziri wa Ndani wa Elimu ya Juu, John Chrysestom Muyingo alisema, “Inaonekana rafiki yangu kasisi hajui msimamo wa serikali. Nitakwenda katika afisi yake na kuzungumza naye. Najua ataelewa ufafanuzi wangu na kubadilisha msimamo wake.” (The East African, Jumatatu, 10/01/2022)

**Maoni:**

Ni jambo la kutiwa shaka kwa vyombo vya habari kupatiliza matamshi yaliyotolewa na Kasisi. Kwa upande mwingine, kujitia upofu kwa uhakika wa dori ya dini katika enzi ya mfumo wa kirasilimali wa kisekula kuwa ni ya kushikamana kiushirikiano. Katika hali ambayo dini imetengwa na kuwa pembezoni pale kunapohusiana na masuala ya uongozi na utawala, lakini hutumika pale ambapo uwiano wa kijamii unapotishiwa. Hivyo basi, dini inatumika kama zana na wale walioko mamlakani ili kutimiza ajenda zao ovu kupindukia.

Watu wengi wameikumbatia dini kwa muktadha wa nami nionekane pia ni mtu wa dini. Mtazamo ambao unashawishiwa na maadili ya kirasilimali ya kisekula ambayo yanachukia dini na matukufu yake. Kwa hiyo, watu wengi wakijumuisha kipote cha wachache watawala hudhihirisha hisia za kidini pale ambapo huona ni muafaka kufanya hivyo, lakini wanabakia kuwa watumwa na wanaoabudu mungu wa kidemokrasia. Mungu ambaye kuwepo kwake kumetokamana na akili zao zenye kikomo! Haishangazi kuwa viongozi wa ‘kidini’ wa leo au zamani ima Waislamu au Wakristo nk. wanazingatiwa kuwa ndio mfano wa kuigwa wa walinganizi wa demokrasia na wanahudumu katika ngazi za juu katika tawala za kidemokrasia!

Natija yake ni Muislamu au Mkriso nk. ima kiongozi au la ambaye anakiri kuwa na mshikamano na mfumo wa kirasilimali wa kisekula sio chochote bali ni mchangiaji katika majanga yasiyoisha yaliyopo yanayoukumba ulimwengu leo. Naam. Kwa sababu kujisalimisha kwao kwa mfumo wa kirasilimali wa kisekula umewafanya kuwa dhaifu na wasiotegemeeka katika kutatua matatizo yayo hayo ambayo yamechipuza kutoka katika kujifunga kwao na mfumo batili wa kirasilimali wa kisekula na kutekeleza nidhamu zake zenye sumu. Hivyo basi, sio jambo kushangaza kuwa na hizi purukushani za sasa nchini Uganda. Mwanzoni alikuwa ni Rais aliyefariki wa Tanzania John Pombe Magufuli ambaye aliipatiliza karata ya maadili, lakini aliridhika na utawala wa kidemokrasia ambao unawapa wanadamu uhuru usiokuwa na mipaka!

Kwa kuhitimisha, tunahitaji wafuasi wa kweli wa dini. Dini ya kweli ambayo inachipuza kutoka kwa Muumba wa ulimwengu, uhai na mwanadamu. Dini ambayo kitabu chake cha muongozo hakijachafuliwa au kuchanganywa ili kukidhi maslahi ya watu binafsi. Dini hiyo ni Uislamu. Uislamu ni mfumo (mwenendo kamili wa maisha) ambao huhitajika kutekelezwa juu ya wanadamu. Ili wanadamu waweze kufurahia amani, utulivu na ustawi ambao wanaouhitaji, lakini hawaja ushuhudia chini ya enzi ya mfumo wa kirasilimali wa kisekula. Hakika, ni Uislamu pekee chini ya nidhamu ya utawala ya Kiislamu ya Khilafah iliyosimamishwa kwa njia ya Utume ndiyo itakayoleta utuli katika nyanja zote za maisha.

Khalifah, Muislamu mwanamume mwenye uwezo na mwenye kujisalimisha katika maamrisho ya Uislamu na kufanya kazi usiku na mchana kuzitekeleza nidhamu za Uislamu. Ni yeye pekee kupitia Khilafah ndiye atakaye rudisha nidhamu na mpangilio katika ulimwengu huu wa fujo wa kirasilimali wa kisekula wenye uhuru usiokuwa na mipaka.

**Imeandikwa kwa ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na**

**Ali Nassoro Ali**
**Mwanachama wa Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**

# Dola ya Tashwishi ya Kirasilimali Ikivalia Vazi la Kiislamu

**Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na**

**Nabil Abdul Karim**



Wakati Ummah ukielekea katika ufahamu wake jumla wa kutoshindikana kurejea kwa Khilafah, tunaona baadhi ya watu wakimtafuta mkombozi kutoka kwa pote la viongozi walio mamlakani, ambaye anafaa zaidi kwa jukumu hili, na wanapendelea Raisi wa Uturuki Erdogan kuwa ndiye mwenye kufaa kwa jukumu hili. Hivyo, wanakubalisha matendo yake yote na kujaribu kuyakuza. Wanafikiri kuwa anatenda kisiri kwa ajili ya kuurejesha Uislamu madarakani, na kurejesha utekelezaji wa Sheria za Mwenyezi Mungu (swt)!

Bali kwa ushujaa wa mbwa mwitu na ujanja wa mbweha, Erdogan anajitahidi kuwalaghai baadhi kwa njia zisizo za moja kwa moja kuwa utekelezaji wa Uislamu unaweza kufanyika hatua kwa hatua, ili kuepuka hasira za dunia zinazopinga kusimamishwa kwa dola ya Kiislamu, na kuepuka uvamizi wa ghafla. Tunaona waungaji mkono wa muelekeo wa Erdogan wakihalalisha utekelezaji wake wa sheria safi za kisekula kuwa ni aina ya udanganyifu kwa Wamagharibi, na kuwa matendo yote anayotenda yanaonyeshwa na serikali yake kuwa anafanya kazi kisiri kuurejesha Uislamu madarakani.

Haya ndiyo yale aliyoyataja mwandishi wa Jordan, Daoud Omar Daoud katika makala kwenye “Al-Quds Al-Arabi” yenye kichwa: “Vita vya Majaliwa na Kurejeshwa kwa Maisha ya Kiislamu,” ambapo alijaribu kuhusisha fikra za Erbakan na ushawishi wake kwa fikra za Hizb ut Tahrir, kama alivyodai. Fikra za Sheikh Taqiuddin An-Nabahani, muasisi wa Hizb ut Tahrir, Mwenyezi Mungu amrehemu, zimetokana na Quran na Sunnah, na kila anayesoma anaathirika nazo kwa sababu ni mtazamo wenye chimbuko la ki-Wahyi unaowakilisha kitulizo kwa majeraha ya Ummah huu na dunia. Hakuna shaka juu ya hilo. Hata hivyo, kubeba fikra ni vigumu kwa sababu madhalimu wote wa dunia wanataka kuzuia utawala wake, na kuibua vita kusitisha utawala wake ukiwa ni muundo wa utekelezaji. Hii ni kwa sababu fikra hizi za Hizb ut Tahrir ni za kipekee katika utekelezaji wa Uislamu zikiwa ni fikra na twariqa (njia), itawaondoa kutoka mizizi yao mara baada ya kuiweka kwenye medani ya kimataifa, inayojumuishwa ndani ya Dola hii kubwa ya Kiislamu ambayo inatumia hukumu za Shariah.

Japokuwa mwandishi ameeleza wazi kuwa Erbakan alitaka kuanzisha muungano wa Kiislamu, shirika la

***Endelea... UK 7***

Umoja wa Mataifa kwa Waislamu, uanzishwaji wa muungano wa kijeshi wa Kiislamu kama wa NATO, utoaji wa dinar ya Kiislamu kuzuia Wamagharibi kutupora, kuanzisha soko la uchumi la pamoja, na kuondoa ushuru, hati za kusafiria na viza baina ya nchi za Kiislamu, yote hayo ni majaribio ya kuunganisha nchi za Waislamu katika umbo maalum katika muundo wa nchi za kirasilimali, kana kwamba hatuna mfumo wa kipekee wa Kiislamu ambao ni tofauti katika muundo wake na mfumo wowote wa kisiasa, ni mfumo wa Khilafah ambao Sheikh Taqiuddin, Mwenyezi Mungu amrehemu, ameuchambua kwa vizuri kwa dalili za kiSharia katika kitabu, Nidhamu ya Utawala. Erbakan alitaka kuunda dola ya Kiislamu iliochanganyika na usekula, ambapo atatumia baadhi ya hukumu za ki Sharia huku akihifadhi muundo wa dola ya kirasilimali. Hata hivyo, usimamishaji wa dola ya Kiislamu una njia ilio wazi katika fikra za Sheikh Taqiudin An-Nabahani, muanzilishi wa Hizb ut Tahrir, Mwenyezi Mungu amrehemu.

Lengo la Erbakan katika majaribio yake ni kuiburuza nchi ikubali usekula unaozunguka ndani ya mzingo wa Ulaya. Uwepo wa Waislamu hawa walioundwa kushiriki katika mfumo huo na kukubali usekula usiopendelea upande wowote na kukubali mchakato wa kidemokrasia, lakini wakati hatari ya ushawishi wa Amerika ilipomjia au kupitia kati yake au kupitia kumtega, kwa sababu Amerika imeunga mkono hatua zake ndefu katika Cyprus, jeshi la Uturuki, katika kujidhalilisha kwa Ulaya, ilikuwa ni hofu kwa tabia ya Erbakan kwa Amerika na mara moja aliivunja serikali yake, ambayo haikudumu kwa zaidi ya miezi 13, na kulazimika kujiuzulu. Hatua hii ilizingatiwa ni moja ya hatua za kushindwa kwa Amerika kuiweka Uturuki kwenye mikono yake, na sio, kama baadhi wanavyodai kuwa aliivunja kutokana na hamu yake ya kutekeleza Uislamu.

Kuja kwa Erdogan madarakani, kuliiwezesha Amerika kuinyakua Uturuki kutoka kwenye makucha ya Uingereza kupitia mapambano makali ya kisiasa, ya mwishoni kabisa ni mapinduzi ya karibuni yaliowezesha kuondoa uwepo wote wa Ulaya katika Uturuki. Lakini kuna vitu katika medani za kimataifa ambavyo vimebadilisha baina ya kipindi cha Erbakan na cha Erdogan. Mwanzoni, Amerika ilitaka kuwavuta maSunni upande wake na kuwaondosha kutoka ndani ya guo la Uingereza, na kwa hivi sasa haya yamepatikana, baada ya kumiliki nchi nyingi za Waislamu, hasa Saudi Arabia, kumaliza Uwahabi, na kubadilisha utiifu wa watawala wa Saudi Arabia kunyenyekea sera ya Amerika, na haya hayakufichikana kwa yeyote hivi leo.

Kama tutachukua kile alichokisema muandishi (japo kinaweza kuwa na sehemu ya uhalali) bila kuleta madhara yoyote, basi kuna uwezekano aina tatu ambao hauna wa nne:

1-Kuwa kile kinachosemwa kuhusu raisi wa Uturuki kufanya kazi ya kurejesha Khilafah na kurejesha tena maisha ya Kiislamu ni kweli. Hili liko mbali na ukweli. Alikuwa waziri mkuu tokea mwaka 2003, na baada ya kuigeuza serikali kuwa ya mfumo wa kiuraisi, aliendelea kutawala kama raisi wa jamhuri tokea 2014. Tunaona kuwa mafanikio yote aliyoyafanya katika Jamhuri ya Uturuki yamefanikishwa kwa usekula na alitamka kwa majigambo na kinywa kipana kwenye mahojiano yake. Na hili ndilo alilolisema katika Kituo cha Al-Arabiya kwenye mahojiano naye miaka minne iliyopita wakati mtangazaji alipomuuliza kuwa wengi wanapata shida kuchanganya Uislamu na usekula, alijibu:

“Ninapata shida ya kuelezea ufahamu wa ulimwengu wa Kiislamu katika kuunganisha Uislamu na usekula, tokea tuanzishe chama chetu na kuufafanua usekula, na tumeelezea mahusiano ya Uislamu na muunganisho wake na ugaidi, hivyo tumetafautisha baina ya kuwa Waislamu kama watu binafsi na mfumo wa kisekula. Mimi ni Muislamu ninayetawala Uturuki kwa mfumo wa kisekula, ambapo humaanisha kuvumiliana kwa serikali. Na serikali inasimama kwa kiwango sawa kwa dini zote na madhehebu. Je hii ni kinyume na Uislamu?” **Mwisho wa nukuu**.

Amelielezea hili kwa uwazi kuwa anatawala kwa mfumo safi wa kisekula na hana nia ya kutekeleza mfumo mwengine japo kuwa yeye ni Muislamu!

Kwa upande mwengine, imepita miaka zaidi ya saba tokea aliposhika nafasi ya Uraisi wa Jamhuri, na kila mwaka tunamuona akiwa mbali zaidi na Uislamu kuliko mwaka wa kabla yake! Katika upande wa kisiasa, tunaona ndege za kivita zikipaa kutokea ardhi yake zikiua Waislamu nchini Syria, Libya na Iraq, na yeye ndiye aliyejenga ukuta mpakani na kuitenganisha na Syria na kumuuwa kila anayejaribu kuuvuka kutoka kwenye majirani zake Waislamu, akitekeleza maagizo ya Amerika kupambana na Uislamu na Waislamu bila kificho, bali ameyaeleza hayo wazi. Kwa bahati mbaya, baadhi ya watu wanaunga mkono kile anachokifanya pamoja na kuthibitisha.

Ama kwa upande wa uchumi, tunafahamu namna alivyopiga pigo la mwisho kupata mafanikio ya kisiasa kabla ya uchaguzi kuwapiga wapinzani wake, hata kama haya yamefanywa kwa kuwapa shida watu na kuwashindisha na njaa. Baada ya kufanya maboresho yenye muelekeo wa riba ya wazi, akiwaitia watu kuweka akiba fedha zao na kuchukua mikopo ya benki yenye riba, kwa mrejesho wa kuwahakikishia mapato kwa msingi wa riba, tukashuhudia bei za kila kitu zikipanda zaidi na zaidi. Malipo ya umeme, gesi na mafuta yameongezeka kwa zaidi ya asilimia 50, na kupanda kwa vitu hivi kumepelekea kuongezeka kwa bei katika namna ya kutisha, yaani, amewapatia zawadi kwa mkono wa kulia na kupokea kutoka kwao mara mbili kwa mkono wa kushoto! Je hii ndio namna ya ushughulikiaji wa mambo ya watu?! Au ni mafanikio maalum katika matayarisho kwa ajili ya uchaguzi ujao wa 2023 kubakia madarakani

***Endelea... UK 8***

huku Amerika ikimuunga mkono na kusimama nyuma yake.

Baada ya uchambuzi huu, tunaona kuwa uwezekano huu uko mbali na ukweli, bali Erdogan anacheza na hisia za hamu ya Ummah ya kurejea kwa Uislamu.

2- Yeye ni Muislamu anayetawala kwa usekula na hana nia ya kuwa Khalifah wa Waislamu, na hafanyi kazi ya kutekeleza sheria za Uislamu. Hapa vile vile, tunaona kama hii ndio hali, matendo yake anayojisifia nayo kwa Uislamu yanaweza kubadilika, kama kauli yake: “Nitaendelea na juhudi zangu kwenye riba hadi nimewatoa watu wangu kutoka kwenye janga hili kubwa,” na kauli yake: “Riba ni sababu, na athari yake ni upandaji wa gharama za maisha.” (Kauli za Erdogan 19/12/2021)

Hapa swali linazuka: Kwa nini tunashuhudia upotoshaji wa Wamagharibi wa taswira ya kila raisi anayedhaniwa kuwa Muislamu sana, na kumfukuza kutoka madarakani mara moja, bila kujali upande aliomtiifu kwake, na hili ndilo lililotokea kwa wengi hata kama walikuwa watiifu kwa mfumo wa kimataifa na kutekeleza maagizo ya Amerika na wengineo, na bado walienguliwa, lakini hatujashuhuia hilo kutokea kwa Raisi Recep Tayyip Erdogan?! Kwa nini?

Unamuona akipanda majukwaa ambayo kwa uwazi yanaunga mkono Uislamu, na anafanya baadhi ya harakati zinazoonyesha Uislamu, hata kama ni kwa uchache, lakini bado hatuoni Amerika ikifanyakazi ya kumuondoa, bali anapata msaada mmoja baada ya mwengine.

Japokuwa kama angechukua au kutekeleza hukumu kwa kile alichoteremsha Mwenyezi Mungu, Ummah wote ungelimfuata mara moja, kwa sababu ya hamu ya unyenyekevu ilionao kwa ajili ya kurejea kwa hukumu za Uislamu na siku za utukufu na heshima. Ummah unasimama upande wa yule anayetaka kutekeleza Shariah na kurejesha maisha ya Kiislamu. Utavitoa muhanga vyote vyenye thamani kwa ajili ya hili. Kama alifikiria na kuchukua hatua moja katika muelekeo huu, angeliona kwa macho yake mwenyewe mandhari kubwa ya Ummah huu mkarimu, lakini hatuoni hatua yoyote ya Amerika dhidi yake, bali tunaona msaada wa kiuchumi, kisiasa na kijeshi na nafasi za kimataifa zinazoinyanyua hadhi ya Uturuki na kuisukuma kwenye nafasi ya nchi kubwa za kiuchumi.

3- Uwezekano wa mwisho, japokuwa natarajia liko nje ya mada, kwa sababu ya ujanja mkubwa unaofanywa dhidi ya Ummah huu. Wamagharibi wanajua kuwa Utawala wa Khilafah Rashidah, Mwenyezi Mungu ajaalie, ni wenye kuja, hivyo wanaleta mtu wa utawala aliye karibu na akili za watu ya kuwa anafaa kuwa Khalifah, lakini yeye yuko mbali na hilo; ambalo linaambatana na tabia za Erdogan, na hiyo ni kwa sababu ya kuficha, inaweza kuwa ni kilango cha salama wakati dola ya kweli ya Khilafah itaposimamishwa, hivyo yeye pia anatangaza kusimamishwa kwa Khilafah ya Kiislamu na kutekeleza Shariah, lakini kwa lengo la kuzuia Khilafah ya kweli na kuhamisha mazingatio, haya yanafahamika kwa watu na yalifanyiwa kazi kabla.

Khilafah ya kweli inaweza kuwa ni mpya katika matukio, na kwa kuwepo kwa nususi za wazi, ikiwemo Hadithi ya Mtume (saw):

إِذَا بُويِعَ لِخَلِيفَتَيْنِ، فَاقْتُلُوا الْآخَرَ مِنْهُمَا

**"Watakapopewa bay’ah makhaifah wawili, basi muuweni wa mwisho wao."**

Hata hivyo, kujiweka mbali kwa watu na Dini kwa miaka zaidi ya mia moja imewapelekea kuwa na udhaifu mkubwa wa kifikra na hawakuyatia mafundisho haya kwenye vitendo.

Shakhsiya ya Erdogan ni yenye kufaa kwa nafasi hii kwa sababu ya ujanja na udanganyifu wake, na wanamuamini sana, kwa kuwa anatekeleza kila kitu kwa usahihi kama anavyotakiwa, wana uhakika kwamba hatousimamisha Uislam hata akipata msukumo wa aina gani, kwa kuwa anafanya kazi ya kutekeleza usekula, anawaruhusu Waislamu kushusha pumzi na kugeuza hisia zao juu ya suala la kuurejesha Uislamu kutawala. Uwepo wake unatengeneza kilango cha salama kwa namna mbili:

1-Kazi yake ya kuunganisha fikra ya usekula na Uislamu, anaoutangaza. Anazingatia Uturuki kuwa ni mfano wa kuigwa, ambayo imefanikiwa kuwa na usawa, haki, neema na maisha ya starehe.

2-Yupo tayari kucheza dori alizopangiwa kuuvunja Uislamu.

**Enyi Waislamu!** Ujanja wa Wamagharibi umezidi ubunifu wote, kwa hakika haupuuzi watu mashuhuri aina hiyo pindi wanapokuwa watiifu, kwa hiyo msidanganyike kwa wasifu wao, na kuweni katika wenye fikra angavu, na kuweni pamoja na wanaotaka kuitekeleza tena Shariah na kurejesha maisha ya Kiislamu. Wajibu huu una njia moja, kutoka kwenye fikra ya Kiislamu yenyewe, ambayo imechorwa na Mtume wetu Mtukufu na yeye (saw) ameonyesha njia safi ambayo tunahitajia kuifuata katika kumtii Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, kuasisi dola ya kweli ambayo Mwenyezi Mungu (swt) ametuahidi, na bishara njema tumeshapewa na Mtume wetu (saw) katika Hadithi tukufu:

ثُمَّ تَكُونُ خِلَافَةً عَلَى مِنْهَاجِ النُّبُوَّةِ

**“Kisha kutakuwa na Khilafah kwa njia ya Utume”.**

Basi fanyeni kazi pamoja na wafanyao na msiwe miongoni mwa wapotezaji wa fursa hii.

# HABARI NA MAONI
# Uislamu ndio Wokovu Pekee kwa Watoto wa Tharparkar

**Habari:**

Ripoti ya kuogofya ya vifo vya watoto zaidi ya 36 katika wilaya ya Tharparkar, vilivyosababishwa na maradhi mbalimbali katika mwezi wa kwanza wa 2022, imesababisha kizungumkuti kwa serikali ya mkoa. (Tribune Pakistan)

**Maoni:**

Kwa mujibu wa rekodi ya Idara ya Afya ya Tharparkar, zaidi ya watoto 600 waliozaliwa walikufa katika mwaka uliotangulia, 2021. Vifo hivi vilitokana haswa na kutopatikana kwa huduma za afya na lishe duni. Kama tunavyojua sote kwamba maisha yanategemea maji, watu wa Thari hutumia sehemu kubwa ya siku yao kutafuta maji safi ya kunywa, na katika hili, usafi wao ni tofauti na usafi wa kawaida.

Kuna vyanzo tofauti wanavyotumia, kama kukusanya maji ya mvua na visima virefu vilivyochimbwa. Kwa sababu ya matumizi ya mara kwa mara ya maji ya ardhini yenye floridi ya juu, maradhi ya fluorosis yamekuwa janga eneo la Thar, na kusababisha fluorosis ya meno, ulemavu wa viungo, na matatizo ya tezi na figo. Hii inasababisha watu wazima wenye utapiamlo kuzalisha na kulea (kama watabakia hai) watoto wenye utapiamlo. Wilaya ya Tharparkar ina wakazi wanaokadiriwa kuwa milioni 1.6, waliosambaa zaidi ya kilomita 22,000 mraba. Uhaba wa maji ni tatizo kubwa la eneo hili. Na visima vilivyochimbwa vimepatikana kuwa chanzo pekee endelevu cha maji ya ardhini. Wamekuwa wakiishi kwa maji yaliyochafuliwa, chumvi na maji ya ardhini ambayo hayajatibiwa. Siku yao huanza kwa kubeba mitungi ya maji, ambayo hujaza kutoka kwa maji ya mvua yaliyohifadhiwa au matangi madogo ya asili, baada ya kutembea zaidi ya kilomita 3 kwenye joto kali.

Serikali tofauti tofauti kwa miaka mingi zimetumia kisiasa ukame, njaa na vifo vya watu wa Thari kwa manufaa yao wenyewe. Miradi ya maji ilitangazwa ambayo haikufikia kukamilika; kutokuwepo kwa vituo vya matibabu huongeza mafuta kwenye moto na kutafuta msaada wa matibabu kunaweza kuwagharimu watu wanaolazimika kutembea umbali mrefu na kutumia pesa nyingi. Mnamo 2021, Mahakama ya Upeo iligundua vifo vya watoto, na iliona kuwa hakuna madaktari, dawa au vituo vya afya vilivyopatikana katika hospitali za Tharparkar, ambayo inaonyesha kukatika kabisa mafungamano ya Serikali na watu.

Watu wa Ummah huu wanahisi uchungu kwa kaka na dada zao na tunaona watu binafsi na mashirika mengi yakifanya kazi kwa ajili ya watu wa Thari. Kambi za matibabu za kibinafsi zimewekwa na watu na msaada pia hutolewa lakini bila shaka hizi haziwezi kukidhi mahitaji. Kwa njia hii watu huishia kulipa gharama mara mbili, kwanza kwa Serikali kwa njia ya kodi na pili kwa kuwasaidia watu wa Thari moja kwa moja. Suala hili linahitaji mpango ufaao na haliwezi kusuluhishwa, Tharparkar ndio jangwa pekee lenye rutuba duniani na kwa mujibu wa uchunguzi wa kijiolojia wa hifadhi ya makaa ya mawe ya Pakistan inakadiriwa kuwa takriban tani bilioni 175, na kuifanya kuwa mojawapo ya hifadhi kubwa zaidi za makaa ya mawe ya lignite Dunia. Endapo hifadhi hizi zitatumiwa kwa uaminifu basi sio tu zinaweza kusaidia kutatua matatizo ya nishati ya Pakistan, vilevile zinaweza kupanga maisha ya utu kwa watu wa Thari. Hata kama hakukuwa na hifadhi ya makaa ya mawe, na kutengeneza mifereji ya maji kwa ajili ya kuwasaidia watu wa Thar haikuwezekana, jukumu la Serikali la kuokoa maisha na riziki za watu wake bado linabakia.

Katika Uislamu, Mtawala ni mmoja kwa Ummah mzima wa Kiislamu, bila kujali rangi au eneo la makaazi. Ni chini ya kivuli cha Khilafah pekee, ndipo tutaona afueni kwa Ummah katika nyanja zote za maisha. Mali za umma zitatumika kwa manufaa ya umma. Khalifah atateua magavana na hao magavana watawajibika kwa eneo lao. Khalifah mwenyewe atafuata mtindo wa Khalifah Umar Bin Al-Khattab aliyeongoka, ambaye kipindi chake cha utawala kilikuwa kirefu zaidi kati ya Makhalifa Waongofu wanne wa mwanzo. Alijulikana sana kwa hisia zake kali za uwajibikaji katika kushughulikia mambo ya Waislamu. Alifanya doria usiku ili kuhakikisha watu wanatunzwa vyema. Mwenyezi Mungu atujaalie mtawala muadilifu. Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) amesema,

مَا مِنْ عَبْدٍ يَسْتَرْعِيهِ اللَّهُ رَعِيَّةً يَمُوتُ يَوْمَ يَمُوتُ وَهُوَ غَاشٌّ لِرَعِيَّتِهِ إِلَّا حَرَّمَ اللَّهُ عَلَيْهِ الْجَنَّةَ

**"Hakuna mja yeyote ambaye Mwenyezi Mungu anamfanya msimamizi wa raia kisha akafa ilhali anawaghushi raia wake, isipokuwa Mwenyezi Mungu amemuharamishia Pepo."** [Al-Bukhari na Muslim]. Riwaya nyengine ni: Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) amesema,

«فَلَمْ يَحُطْهَا بِنُصْحِهِ لَمْ يَجِدْ رَائِحَةَ الجَنَّةِ» **"Kisha asiangalie mambo yao kwa wema na ikhlasi, hatanusa harufu ya Pepo."** Riwaya ya Muslim ni: Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) amesema,

مَا مِنْ أميرٍ يلي أمور المُسْلِمينَ، ثُمَّ لا يَجْهَدُ لَهُمْ وَيَنْصَحُ لَهُمْ، إِلاّ لَمْ يَدْخُلْ مَعَهُمُ الْجَنَّةَ **"Hakuna kiongozi yeyote, anayetawala mambo ya Waislamu, asijizatiti kwa ajili yao na asiwatumikie kwa ikhlasi, isipokuwa hataingia pamoja nao Peponi."**

**Ikhlaq Jehan**

JIBU LA SWALI

# Kwa Nini Mtume (saw) Hakuomba Nusra (Nguvu za Kimada) kutoka kwa Maquraish



**Swali:**

Kwa ajili ya ufafanuzi wa swali: Je, Mtume (saw) kutokuomba kwake Nusra kutoka kwa Maquraish ni kwa sababu hawakuwa na vigezo hivyo kabisa, au ni kwa sababu tu waliukataa Uislamu? Na ninaokusudia ni viongozi wa Makkah. Na ikiwa ni hivyo, si Mtume (saw) aliomba Nusra kutoka kwa watu wa Yathrib [Madina] pamoja na kwamba viongozi wa Yathrib walikuwa hawajasilimu na hawakutoa nusra?! Naomba ufafanuzi.

Mwenyezi Mungu akubariki na akulipe kila la kheri.

**Jibu:**

Kuhusu kutokuomba Nusra kutoka kwa Maquraish wa Makkah, mas`ala ni kama ifuatavyo:

[Mtume (saw) alikuwa akiwalingania wenye nguvu, walio na uwezo wa kubadilisha ujahiliya na kuweka Uislamu, alikuwa kwanza huwalingania kwenye Uislamu ... wakisilimu na kukubali, basi huomba Nusra yao baada ya hapo... na viongozi wa Kiquraishi hapo Makkah wenye uwezo wa kubadilisha hawakuubali Uislamu, ndio sababu Mtume (saw) hakuomba Nusra yao, bali Mtume (saw) alikuwa akitosheka tu na kulingania kwenye Uislamu huko Makkah. Na kwa kuwa wenye nguvu miongoni mwao hawakuitikia Uislamu ndio maana hakuomba Nusra kutoka kwao... hapa chini nitakutajia kutoka kwa Seerah ni vipi hayo mambo yalivyokuwa:

**Kwanza: kutoka kwenye Seerah ya Ibn Hishaam:**

1- [(... na watu wake walikuwa wakali zaidi katika kumkhalifu na kutengana na dini yake isipokuwa wachache tu katika wanyonge waliomuamini. Basi Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) akawa akijionyesha kwa makabila ya Waarabu kwenye misimu [ya hajj], akiwalingania kwa Mwenyezi Mungu, na kuwaeleza kwamba yeye ni nabii aliyetumwa, na akiwaomba wamkubali na wampe ulinzi ili aweze kuwabainishia yale ambayo Mwenyezi Mungu amemtuma nayo...

Amesema Ibn Ishaq: amenihadithia Hussein bin Abdillah bin Ubaidillah bin Abbas: asema, nilimskia Rabia bin Abbaad akimhadithia babangu na kusema: mimi nilikuwa kijana barobaro nikiwa pamoja na babangu huko Minaa, hali ya kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu alikuwa akisimama kwenye mashukio ya makabila ya Waarabu akiwaamba: Enyi bani fulani... hakika mimi ni mjumbe wa Mwenyezi Mungu kwenu, amewaamrisha mumuabudu Mwenyezi Mungu na wala msimshirikishe na chochote, na mvue vyote mnavyoviabudu kutokana na haya masanamu, na muniamini na munikubali, na mnipe ulinzi ili niweze kubainisha kutoka kwa Mwenyezi Mungu yale aliyonituma nayo...)

2- Amesema Ibn Ishaq: na amenihadithia Az-Zuhriy kwamba, [Mtume] aliwaendea Bani Aamir bin Swa`swa`ah akawalingania kwa Mwenyezi Mungu Azza wa Jalla na akajitambulisha kwao. Mtu mmoja kati yao -akiitwa: Baihara bin Firaas. Amesema ibn hIshaam:

***Endelea... UK 11***

Firaas bin Abdillah bin Salamat al-Khair, bin Qushair, bin Ka`ab, bin Rabiiaah, bin Aamir bin Swa`swa`ah - akamwambia: “Naapa kwa jina la Mwenyezi Mungu lau nitamchukua huyu kijana wa Kiquraishi basi ningeliwala (ningeliwashinda) Waarabu kupitia kwake”! Kisha akasema: waonaje ikiwa sisi tutakupa bay`ah [kiapo cha utiifu] juu ya jambo lako, kisha Mwenyezi Mungu akupe ushindi dhidi ya waliokukhalifu, je hili jambo [la utawala] litakuwa kwetu baada yako? Akajibu [Mtume]: hilo jambo ni la Mwenyezi Mungu, na huliweka mahali anapotaka. Akamwambia: hivi shingo zetu zilengwe na Waarabu kwa ajili yako, kisha Mwenyezi Mungu akishakupa ushindi hilo jambo [utawala] liwe kwa wengine?! Hatuna haja na jambo lako...

3- Amesema tena Ibn Ishaq: “Akawa Mtume wa Mwenyezi Mungu ni mwenye kuendelea na jambo lake hilo kila anapokusanyika na watu katika misimu, huwaendea na kuyalingania makabila kwa Mwenyezi Mungu na kwenye Uislamu, na huionyesha nafsi yake kwao [hujitambulisha] na yale aliyo kuja nayo kutoka kwa Mwenyezi Mungu: uongofu na huruma. naye hasikii kuna mtu yeyote amekuja Makkah katika Waarabu na akawa ni mwenye jina [mtambulika] na ubora, isipokuwa humfuata na kumlingania kwa Mwenyezi Mungu, na kumuonyesha aliyo nayo”.

Na kama unavyoona, Mtume (saw) alikuwa akimlingania kwenye Uislamu kwanza mwenye nguvu, akikubali ndipo huomba Nusra yake.

**Pili: kutoka kwenye Seerah ya Ibn Kathir:**

1- [... amesema: kisha tukaishia kwenye mkao wenye utulivu na heshima. Mara [tukakutana na] wazee wenye vyeo, Abubakar akatangulia, akasalimia - amesema Ali: “Na Abubakar alikuwa wa mbele katika kila jambo la kheri” - akawaambia: mwatokana na nani? Wakasema: twatokana na Banu Shaibaan bin Thaalaba. Abubakar akamgeukia Mtume wa Mwenyezi Mungu na kumwambia: nakufidia kwa babangu na mamangu! Baada ya hawa hakuna watu wengine wenye utukufu kuwaliko. Na katika mapokezi mengine: nyuma ya hawa udhuru wowote katika watu wao, na hawa ni wa mbele katika watu wao, hawa ni viongozi wa watu! Na kati yao walikuwepo Mafruq bin Amr, Hani`i bin Qubaiswa, Muthanna bin Haritha, na Nu`maan bin Harik... na aliyekuwa karibu zaidi kwa Abubakar ni Mafruq bin Amr. Na alikuwa huyu Mafruuq bin Amr amewashinda kwa ufasaha, na alikuwa na misuko miwili ya nywele iliyoangukia kifuani kwake, na ndiye aliyekuwa karibu sana kwa Abubakar katika mkao. Abubakar akamuuliza: idadi yenu iko vipi? Akajibu: hakika sisi twazidi elfu moja, na hawatoshindwa watu elfu kutokana na uchache. Akamuuliza tena: na nguvu yenu ikoje? Akajibu: ni juu yetu kujitahidi, na kila watu hujikakamua. Abubakar akamuuliza: na vita kati yenu na maadui zenu huwa vipi? Mafruq akajibu: sisi huwa wakali zaidi pale tunapokasirika, na hakika sisi hufadhilisha farasi kuliko watoto, na silaha kuliko mashamba, na ushindi hutoka kwa Mwenyezi Mungu, mara nyengine hutupa ushindi na mara nyengine huwapa ushindi wengine dhidi yetu... huenda wewe ni ndugu wa Maquraish? Akasema Abubakar: ikiwa mumefikiwa na habari kuwa kuna Mtume wa Mwenyezi Mungu basi huyu hapa ndiye. Akasema Mafruq: imetufikia kwamba anasema hivyo. Kisha akamgeukia Mjumbe wa Mwenyezi Mungu na kumuuliza: walingania nini ewe ndugu wa Maquraish? Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) akatangulia mbele, akaketi, na Abubakar akasima na kumuekea kivuli kwa nguo yake. Akasema Mtume (saw):

**أدعو إلى شهادة أن لا إله إلا الله وحده لا شريك له وأني رسول الله وأن تؤووني وتنصروني فإن قريشا قد تظاهرت على أمر الله وكذبت رسله واستغنت بالباطل عن الحق والله هو الغنى الحميد**

“**Nawalingania kwenye kushuhudia kwamba, hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu, peke yake na hana mshirika, na kwamba mimi ni Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, na munihifadhi na muninusuru ili niweze kufikisha [ujumbe] wa Mwenyezi Mungu alioniamrisha, kwani Maquraish wameshirikiana dhidi ya amri za Mwenyezi Mungu, na wakamkadhibisha Mjumbe wake, na wakatosheka na batili badala ya haki, na Mwenyezi Mungu ndiye Mkwasi na Mwenye kusifiwa**”. Akamuuliza tena: na walingania nini tena, ewe ndugu wa Maquraish? Mtume wa Mwenyezi Mungu akawasomea:

**قل تعالوا أتل ما حرم ربكم عليكم: ألا تشركوا به شيئا وبالوالدين إحسانا**

**"Sema: Njooni nikusomeeni aliyo kuharimishieni Mola wenu Mlezi. Nayo ni kuwa, msimshirikishe Yeye na chochote. Na wazazi wenu wafanyieni wema." Mpaka neno lake: (ذلكم وصاكم به لعلكم تتقون) "Hayo amekuusieni ili myatie akilini."** [Al-An'am: 151]

Mafruq akasema: “Na walingania nini tena, ewe ndugu wa Maquraish? Naapa kwa jina la Mwenyezi Mungu haya si maneno ya watu wa ardhini, na lau ingekuwa ni katika maneno yao basi tungelijua!” Mtume akamsomea:

**إن الله يأمر بالعدل والإحسان وإيتاء ذى القربى وينهى عن الفحشاء والمنكر والبغى، يعظكم لعلكم تذكرون**

**"Hakika Mwenyezi Mungu anaamrisha kufanya uadilifu, na hisani,na kuwapa jamaa; na anakataza uchafu, na uovu, na dhulma. Anakuwaidhini ili mpate kukumbuka."** [An-Nahl: 90]

Mafruuq akamwambia: “Wallahi umelingania -ewe ndugu wa Maquraish - kwenye tabia njema na matendo mazuri, na kwa hakika wamezua uongo watu ambao wamekukadhibisha na wakaungana dhidi yako”!

Na ni kana kwamba alipenda Hani`i bin Qubaiswa ashirikiane naye katika mazungumzo, akasema: “na huyu ni Qubaiswa bin Hani`i mzee wetu na mwenye dini

***Endelea... UK 12***

yetu. Hani`i akasema: “Hakika nimesikia maneno yako, ewe ndugu wa Maquraish, na nimeyakubali, na mimi naona suala la sisi kuacha dini yetu na kufuata dini yako kwa kikao kimoja tu ulichokaa na sisi ambacho hakina mwanzo wala mwisho, na bado hatujafikiria kuhusu jambo lako na kuangalia mwisho wa unayotulingania, [kufanya hivyo] ni kuteleza katika rai, na ni ukurupukaji katika akili, na pia ni uchache wa kuangalia mwisho wa mambo, na hakika si vyengine kuteleza hutokana na uharaka. Na nyuma yetu kuna watu ambao twachukia kuwaamulia jambo, lakini wewe rudi na sisi tutarudi, wewe kayaangalie na sisi tuyaangalie”.

Naye ni kama alipenda Muthanna ashirikiane naye katika mazungumzo, akasema: “na huyu ni Muthanna, mzee wetu na mwenye kuhusika na vita vyetu”. Muthanna akasema: “Bila shaka nimeskia maneno yako na nimeyaona ni mazuri ewe ndugu wa Maquraish, na nimeyapenda uliyozungumza, na jibu ni lile lile jibu la Hani`i bin Qubaiswa, na sisi kuachana na dini yetu na kukufuata kwa kikao kimoja tu ulichokaa na sisi... na hakika sisi tumeshukia katika sehemu mbili za maji: moja wapo ni “Yamama”, na nyengine ni “Samaawa”. Mtume (saw) akamuuliza: ni zipi hizo sehemu mbili? Akasema: “moja wapo ni ... nchi kavu na ardhi ya Waarabu, na nyengine ni ardhi ya Fursi na mito ya Kisra. Na sisi tumeshukia kwa ahadi aliyochukua kwetu Kisra kwamba tusizushe jambo, wala tusimhifadhi mzushi, na huenda hili jambo ambalo watulingania ni miongoni mwa mambo yanayochukiwa na wafalme, ama [sisi kukupa ulinzi] sehemu zinazokaribiana na miji ya Waarabu, hilo ni kosa ambalo mwenyewe aweza kusamehewa, na udhuru wake utakubalika, ama zile sehemu zinazokaribiana na miji ya Wafursi, basi ni kosa lisilosamehewa, na udhuru wake haukubaliki. Kwa hiyo, kama utataka tukunusuru na tukulinde kwa sehemu za Waarabu basi tutafanya hivyo”.

Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) akasema:

ما أسأتم في الرد إذ فصحتم في الصدق وإن دين الله لن ينصره إلا من حاطه من جميع جوانبه

**“Hamjatoa jibu baya, kwa sababu mumesema ukweli kwa ufasaha, [lakini] hatoisimamia dini ya Mwenyezi Mungu isipokuwa yule atakayeizunguka kwa pande zake zote”...]**

2- Asema: [kisha tukaondoka na kwenda kwenye mkao wa Aus na Khazraj, basi hatukuenuka hapo mpaka wakampa Bay`ah Mtume (saw).

Ali (ra) alisema: “Na walikuwa wakweli na wenye subra, basi Mtume (saw) akafurahishwa sana kutokana na Abubakar kujua nasaba zao”.

Asema: “Basi Mtume (saw) hakukaa isipokuwa kidogo tu mpaka akawatokea maswahaba zake na akawaambia:

احمدوا الله كثيرا، فقد ظفرت اليوم أبناء ربيعة بأهل فارس، قتلوا ملوكهم واستباحوا عسكرهم وبي نُصروا

**“Msifuni Mwenyezi Mungu kwa wingi, kwani kwa hakika leo wana wa Rabiiah wamewashinda watu wa Fursi, wamewaua wafalme wao na wakachukua kambi zao, na ni kwa ajili yangu ndio wamenusuriwa.”**

Akasema: “na hilo tukio [la vita] lilikuja kutokea huko “Qaraqir” pambizoni mwa “Dhii Qaar”... na hii ni hadith “Gharib jidda” [geni sana] tumeiandika kwa kuwa ndani yake kuna dalili za utume, tabia njema, na ufasaha wa Waarabu. Na hii [hadith] imekuja kwa njia nyengine, na ndani yake imekuja: kwamba wao [Waislamu] walipopigana na Wafursi na kukutana nao huko “Qaraqir” ambapo ni karibu na “Furaat” walifanya kauli mbiu yao ni jina la Muhammad (saw) ,wakapewa ushindi dhidi ya Wafursi kwa hilo. Na baada ya hilo [Wafursi] waliingia katika Uislamu.

Na imam Muhammad bin Umar Al-Waqidiy amefuatilia kwa undani akasimulia yale makabila moja baada ya nyengine, akataja kujitambulisha kwake (saw) kwa: Bani Aamir, na Ghassaan, Bani Fazaarah, Bani Murra, Bani Hanifa, Bani Sulaim, Bani Abasa, Bani Nadhr bin Hawaazin, Bani Thaalaba bin Ukaba, Kinda, Kalb, Bani Al-Haarith bin Kaab, Bani Udhra, Qais bin Al-Hatwim, na makabila mengine. Na mtiririko wa habari zao ni mrefu, tumetaja miongoni mwa hizo habari kiasi kinachofaa, sifa njema na wema zote ni za Mwenyezi Mungu.

Na amesema Imam Ahmad: ametuhadithia As`wad bin Aamir, [akisema] alitueleza Israil, kutoka kwa Uthmaan -yaani - bin Al-Mughirah, kutoka kwa Salim bin Ja`ad, kutoka kwa Jaabir bin Abdillah, akisema: “alikuwa Mtume (saw) akijionyesha nafsi yake [akijitambulisha] kwa watu kwenye kisimamo cha Arafah, kwa kusema:

هل من رجل يحملني إلى قومه فإن قريشا قد منعوني أن أبلغ كلام ربى عز وجل؟

**“Je, kuna mtu ambaye atanichukua mimi na kunipeleka kwa watu wake? Kwani Maquraish kwa hakika wamenizuia kufikisha maneno ya Mola wangu Mtukufu?”]**

Ni wazi kutokana na [nukuu zote hizo] kwamba, Mtume (saw) alikuwa haombi Nusra kutoka kwa yeyote isipokuwa baada ya kumlingania kwenye Uislamu, na ikiwa hakuitikia Uislamu basi hakuomba Nusra yao.

**Ndugu Yenu,**

**Ata Bin Khalil Abu Al-Rashtah**

**26 Jumada Al-Awwal 1443 H**

**30/12/2021 M**